# Eneo la Uhuishaji na Uboreshaji wa Jiji (CRIZ)

## Kifurushi cha Kuwasilisha Ripoti na Taarifa 2025

Kwa Mwaka wa Taarifa Januari 1 - Desemba 2025 ,31

Mwisho wa kuwasilisha ni kabla au ifikapo tarehe 2026 ,15










ErieCRIZ
City Revitalization & Improvement Zone

# Eneo la Uhuishaji na Uboreshaji wa Jiji (CRIZ) ni nini?

Eneo la Uhuishaji na Uboreshaji wa Jiji (CRIZ) lilianzishwa na sheria ya jimbo mwaka 2013, kwa lengo la kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kufufua baadhi ya maeneo ndani ya mji. CRIZ inajumuisha takribani ekari 130 katikati ya jiji la Erie pamoja na maeneo mengine ndani ya jiji yaliyoteuliwa.
Kwa mujibu wa sheria, sehemu ya kodi za serikali ya jimbo na za ndani zinazokusanywa kutoka kwa biashara zilizopo ndani ya CRIZ, wakiwemo wakandarasi wa miradi ya CRIZ, yanaweza kutumika kufadhili miradi ya maendeleo ya kiuchumi.
Mwaka wa mwanzo (baseline year) ni mwaka ambao eneo hili liliidhinishwa. Kwa Erie, mwaka wa mwanzo ni 2024.

Eneo hili la CRIZ linasimamiwa na Mamlaka ya Erie CRIZ. Mamlaka hii hukutana kila Jumatano ya tatu ya mwezi saa 9 mchana mahali hapa, 100 State Street, Suite 700, Erie, PA 16507. Kwa taarifa zaidi, ikiwa ni pamoja na kufahamu kuhusu taarifa za mkutano huo, tembelea tovuti ya mamlaka ya CRIZ: https://eriecriz.org

## Ili kujua kama biashara yako ipo ndani ya CRIZ, tumia ramani hii:

https://tinyurl.com/ErieCRIZmap

## Bonyeza kwenye ramani ya CRIZ kisha ingiza anuani ya mtaa husika.



# Kwanini CRIZ iliundwa?

CRIZ iliundwa ili kuchochea ukuaji wa kiuchumi wa baadhi ya maeneo kama Jiji la Erie kwa kurejesha sehemu ya kodi za jimbo na za ndani kwenye mamlaka za jiji ili kusaidia kufadhili miradi ya maendeleo na ujenzi mpya.

Kama unamiliki biashara au jengo au vyote kwa pamoja ndani ya eneo la CRIZ, shughuli zako za kibiashara zitachangia ukuaji wa jamii inayokuzunguka iwapo utajaza na kuwasilisha ripoti za kila mwaka kwa siri kwa mamlaka za jimbo na za eneo lako ili kuhakikisha kuwa kodi zinazokidhi vigezo zinafahamika na kurejeshwa kwa Jiji la Erie. Baada ya muda kupita, maeneo yaliyo ndani ya CRIZ yanatarajiwa kuwa na maendeleo zaidi jambo ambalo litaleta ajira mpya, kupunguza majengo yasiyotumika, kuongeza wateja na kuboresha usalama na usafi.

Mpango wa CRIZ ni uwekezaji wa muda mrefu unaofanywa na Jimbo, Jiji, biashara zake na wamiliki wa majengo ndani ya Erie ili kuboresha ustawi wake wa kiuchumi.

## Faida za CRIZ kwa Jiji la Erie:

- Kuongezeka kwa biashara mpya, utalii na makampuni mapya
- Ajira mpya
- Kuwa na jamii imara na shirikishi
- Makazi mengi ya kuchagua
- Mji unaovutia na wenye shughuli nyingi za kuvutia kibiashara
- Ukuaji unaohamasisha matumizi mbalimbali ya ardhi huku maeneo yaliyo wazi na makumbusho ya kihistoria yakihifadhiwa

## Faida za CRIZ kwa Biashara Yako:

- Fursa ya kupata ufadhili wa miradi midogo ili kukuwezesha kuboresha au kukuza biashara yako kama ipo ndani ya eneo la CRIZ
- Kuongezeka kwa imani ya wawekezaji
- Thamani ya majengo kuongezeka iwapo unamiliki jengo ndani ya jiji
- Usalama na miundombinu kuwa bora
- Wateja kuongezeka kutokana na:
    - Kuwa na wageni na watalii wengi wanaotembelea mji
    - Kuwa na hoteli, migahawa na maduka mapya au yaliyoboreshwa
    - Watu wengi wanaofanya kazi ndani ya eneo la CRIZ wanaoweza kuwa wateja

# Uwasilishaji wa Ripoti za CRIZ - Unatakiwa kufanya nini?

Hakuna kodi mpya inayotozwa kwa wamiliki wa biashara na majengo na wakandarasi wanaofanya kazi zao ndani ya eneo la CRIZ katika mpango huu. Hata hivyo, katika sheria ya CRIZ, unatakiwa kuwasilisha ripoti ya kodi ambazo biashara yako tayari huwa inazilipa kwenye mamlaka za jimbo na za eneo lako. Tafadhali anza kujaza fomu zako za CRIZ mapema kabla ya tarehe ya mwisho ya kuziwasilisha.

## NINI

Unachotakiwa kufanya ni kuripoti **MALIPO YALIYOFANYIKA**... hii inamaanisha kwamba unaripoti kile ambacho kimelipwa na biashara yako kuanzia Januari 2025 ,1 hadi Desemba 2025 ,31, bila kujali yalikuwa ni malipo ya mwaka gani wa kodi. Unapaswa kujaza na kutuma fomu zote za mwaka 2025 kwa Idara ya Mapato ya Pennsylvania (DOR) na Ofisi ya Jiji la Erie (COE) kabla au siku ya tarehe 15 Juni, 2026.
Tafadhali anza mapema kujaza ripoti hizi kabla ya tarehe ya mwisho iliyotajwa hapo juu na uweke kumbukumbu za kuwa umetuma ripoti hizi ndani ya wakati.
Unaweza kupata msaada kama ukihitaji—angalia ukurasa wa 9.

Hapo chini kuna orodha ya ripoti zote za kodi za CRIZ zinazohitajika kujazwa. Tafadhali angalia ukurasa unaofuata ili kuona jedwali kamili la kodi za jimbo na za eneo lako zinazohusika.

### Fomu za Jimbo la Pennsylvania (Idara ya Mapato) – JIMBO:

1. Ripoti ya Kodi za Programu ya Eneo la CRIZ – NI LAZIMA IJAZWE NA KUTUMWA KWA NJIA YA MTANDAO

**Mfumo wa kukuwezesha kuiwasilisha mtandaoni utaanza kupatikana kuanzia Aprili 1 hadi Juni 2026 ,15 kupitia:**
https://www.eservices.revenue.pa.gov/NizCriz/Keystone/Session/Login

Hivi karibuni Idara ya Mapato imeanza kutumia mfumo wa usimamizi wa akaunti wa Keystone Login kwa ajili ya kufungulia ripoti ya Jimbo ya CRIZ. Mfumo uliokuwa ukitumika awali wa e-TIDES kwa ripoti za kila mwaka za CRIZ, umeondolewa rasmi. Kama bado haujafungua akaunti yako kwenye Keystone Login, utahitajika kujisajili kabla ya kutuma ripoti yako ya CRIZ ya mwaka huu. Baada ya kuziwasilisha na kabla haujatoka ndani ya mfumo, hakikisha unachapisha uthibitisho wa fomu zako za jimbo ulizowasilisha ili kuweka kwenye kumbukumbu zako.

Tembelea tovuti ya Idara ya Maendeleo ya Jamii na Uchumi wa CRIZ hapa:
https://dced.pa.gov/programs/city-revitalization-improvement-zone-criz/

### Fomu ya Jiji la Erie – ENEO LAKO

1. Ripoti ya Kodi za Ndani ya Mpango wa CRIZ – Jiji la Erie – LAZIMA IWASILISHWE KWA NJIA YA MTANDAO

**Mfumo wa kukuwezesha kuiwasilisha mtandaoni utaanza kupatikana kuanzia Aprili 1 hadi Juni 2026 ,15 kupitia:**
https://crizlocalreporting.eriecriz.org

# Muhtasari wa Kodi Zinazohusiana na Mpango wa CRIZ - Erie

Kodi za jimbo na za eneo lako zimeorodheshwa chini.

Kutoka kwenye orodha ya kodi hizi, angalia na uchambue ni kodi zipi ambazo biashara yako imezilipa tayari (cash basis) mwaka 2025 kisha ziripoti kwenye fomu husika.

## 1 JIMBO
## Kodi za Jimbo la Pennsylvania (Idara ya Mapato):

| | | Tazama Mfano |
|---|---|---|
| 1 | Fomu ya Ziada ya Mgawanyo wa Kodi (kama inahitajika) | APP |
| 2 | Kodi ya Mapato Halisi ya Kampuni * | CNI |
| 3 | Kodi ya Hisa za Benki * | BNK |
| 4 | Kodi ya Malipo ya Bima * | IPT |
| 5 | Kodi ya Mauzo na Matumizi – E-TIDES/Kodi ya Makazi ya Hotelini | SU & HO |
| 6 | Kodi ya Zuio la Mwajiri - Inahusisha Miradi ya CRIZ | Mradi wa EWH & EWH-CRIZ |
| 7 | Kodi ya Pombe Kali au Bia Inayokatwa na Mtengenezaji | MALT |
| 8 | Kodi ya Mauzo na Matumizi Inayolipwa na Mkandarasi kwa Ajili ya Vifaa vya Mradi Eneo la Mpango Huu | C-SU |
| 9 | Kodi ya Mauzo na Matumizi ya Majengo Binafsi au Huduma za Kushikika Zinazotumika na Biashara kwenye Eneo | TPP |
| 10 | Kodi ya Kupitisha ya PIT - Haijumuishi Mapato yasiyohusisha Utendaji wa Moja kwa Moja - Inajumuisha Miradi ya CRIZ | PIT |
| 11 | Jumla ya Kodi Inayohusishwa na Vinywaji vya Ngano au Pombe Zilizonunuliwa ili Kuuzwa tena kwenye Eneo la Mpango Huu (Ushuru na Kodi ya Mauzo) | MALT EX+SLS |
| 12 | Jumla ya Kodi Zinazohusika na Pombe Kali/Mvinyo Ulionunuliwa ili Kuuzwa Tena kwenye Eneo la Mpango Huu (Ushuru na Kodi ya Mauzo) | LIQR |

* Inategemea na Ugawaji. Kodi zingine zote hutumia Ugawaji huo.

## 1 MTAANI
## Kodi za Ndani ya Jiji la Erie:

| | | Tazama Mfano |
|---|---|---|
| 1 | Ujira wa Mwajiri wa Eneo lako | Mradi wa EIT & EIT-CRIZ |
| 2 | Kodi ya Mapato Yaliyopatikana | Mradi wa EIT & EIT-CRIZ |
| 3 | Kodi ya Huduma za Eneo Lako | Mradi wa LST & LST-CRIZ |
| 4 | Kodi ya Burudani | AMT |

# Mchakato wa kuwasilisha ripoti za CRIZ unafanyaje kazi?

MWAKA WA KWANZA: 2025




ErieCRIZ
City Revitalization & Improvement Zone

# Uwasilishaji wa Ripoti ya CRIZ - lini inahitajika na kwanini?

## LINI

Ni lazima ipokelewe kabla au ifikapo tarehe 15 Juni, 2026 kwa mwaka kalenda ulioisha Desemba 2025 ,31 (kuanzia Januari 2025 ,1 hadi Desemba 2025 ,31). Fomu zilizojazwa hazitapokelewa na Mamlaka ya Mapato au na Jiji la Erie baada ya Juni 2026 ,15 (mifumo yao inafungwa baada ya saa 5 na dakika 59 usiku wa tarehe 2026 ,15). Wale ambao hawatawasilisha kwa wakati watatozwa fedha ya adhabu, na jamii ya jiji la Erie haitaruhusiwa kutumia mapato hayo kwa uhuishaji, hivyo tafadhali usichelewe. Tafadhali hifadhi nakala ya ripoti zako za JIMBONI na za ENEO LAKO LA KARIBU ulizojaza kwa kumbukumbu.

Erie CRIZ
Sheria Ilitungwa
(2025)

Mwaka wa Mwanzo

MALIPO YA FEDHA TASLIMU
Kipindi cha Kuripoti 2025
(Januari 2025 ,1 – Desemba 2025 ,31)

Mwisho wa Kuwasilisha Ripoti ni ifikapo au kabla ya Juni 2026 ,15

Uwasilishaji wa ripoti ya CRIZ unapaswa kufanyika kwa mamlaka za jimbo (kielektroniki mtandaoni) na kwa mamlaka za maeneo ya karibu na wewe (zinazojazwa kwa mkono) kwa mwaka wa kalenda 2025.

Oktoba 2026 ,15

Mamlaka za kodi za jimbo na zile za eneo lako zitathibitisha kiasi kilichoripotiwa katika mwaka wa kalenda wa 2025.

Ndani ya siku 10 baada ya kupokea uthibitisho

Ofisi ya Bajeti inamuelekeza Mtunza Hazina kuhamisha fedha zilizothibitishwa kwenda CRIZ.

## KWANINI

Ili mamlaka za kodi za jimbo na za eneo ulipo ziweze kuthibitisha kiasi cha kodi kilicholipwa ambacho Mamlaka ya Erie CRIZ inaweza kutumia kufadhili eneo la CRIZ lenye miradi ya maendeleo.

## Je, ufanye nini kama ukiwa na maswali na ukahitaji msaada?

Tuko tayari kukusaidia. Hivi ndivyo unavyoweza kuwasiliana na sisi:

- Weka miadi ya kufika ofisini kwetu. Tunaweza kukusaidia kujaza na kuwasilisha fomu zako BURE.
- Wasiliana na Deana Zosky, anahusika na kuhakikisha taratibu za CRIZ zinafuatwa na unaweza kumuuliza swali lolote kuhusu namna ya kutuma ripoti yako kupitia barua pepe deana@four-score.com. FourScore ni mshauri aliyeajiriwa na Mamlaka kuwasaidia wafanya biashara kwa mahitaji yao ya kuwasilisha ripoti.
- Wasiliana na nambari yetu ya simu kwa msaada kuhusu kodi kupitia 1289-951-484 au Eriecrizcompliance@four-score.com ambapo mtaalamu wa masuala ya kodi atakujibu maswali yako. Tafadhali acha ujumbe wako kama usipotupata moja kwa moja na mtaalamu wetu atakujibu ndani ya masaa 24.

Tafadhali wasiliana nasi ili tuweze kukusaidia kukamilisha uwasilishaji wa ripoti za CRIZ. Asante kwa kuwa sehemu ya kuhuisha jiji la Erie!

**Fomu ya Ziada ya Mgawanyo wa Kodi ya Makampuni kwa Mwaka 2025**

**Mfano Company, Inc.**

Mfano APP

| | | | |
|---|---|---|---|
| **A. Kipengele cha Majengo** | *Wastani wa Mali Zilizo Kwenye CRIZ 3,000,000 / *Wastani wa Mali za PA 10,000,000 | = | 0.300000 |
| **B. Kipengele cha Mishahara** | Mshahara Ndani ya CRIZ 760,000 / Mshahara wa PA 1,210,000 | = | 0.628099 |
| **C. Kipengele cha Mauzo** | Mauzo Ndani ya CRIZ 2,000,000 / Mauzo ya PA 6,000,000 | = | 0.333333 |
| **D. Jumla ya Ugawaji** | | | 1.261432 |
| **E. Asilimia ya Kodi** | 1.261432 / 3 | = | 0.420477 |
| | | | |
| | | | |
| **E. DENI LA KODI LA CRIZ** | Mstari A – Maeneo Yote ya Pennsylvania X 0.420477 = Sehemu ya CRIZ | | |
| | | | |

**KUMBUKA: Kama kampuni ipo ndani ya CRIZ lakini ina tawi eneo lingine, au ina mali, inatoa mishahara au kufanya mauzo nje ya eneo la CRIZ, basi Fomu ya Ziada ya Mgawanyo wa Kodi iliyopo hapo juu ni lazima ijazwe ili kukokotoa kiasi cha kuripoti kwenye SAFU B (Sehemu ya Eneo lilipo CRIZ).**

*** Wastani wa Mali ni thamani mwanzoni mwa mwaka pamoja na thamani ya mwisho wa mwaka ikigawanywa kwa 2**

# Ratiba ya Malipo ya Kodi Halisi ya PA ya Mapato ya Kampuni ya Mwaka 2025

**Mfano Company, Inc.**

**Kodi Halisi ya Kampuni Iliyolipwa Kuanzia 1/1/2025 hadi 12/31/2025**

Mfano
CNI

Mfano Company, Inc. ina matawi kwenye maeneo kadhaa ndani ya Pennsylvania; matawi mawili yapo ndani ya eneo la CRIZ. Mwezi Machi 2025 walilipa $5,000 kama Kodi Halisi ya Mapato kwenye marejesho yao ya kodi ya mwaka 2024. Pia walilipa Kodi ya Mapato ya Kampuni ya robo mwaka iliyokadiriwa kuwa $60,000 kwa mwaka mzima.

***KUMBUKA: Ripoti hii imeandaliwa kwa kuzingatia pesa taslimu iliyolipwa. Kiasi kinaripotiwa katika kipindi ambacho kinalipwa, sio wakati kinapotakiwa kulipwa.***

**KUMBUKA: Kama kampuni ipo ndani ya CRIZ lakini ina tawi eneo lingine, au ina mali, inatoa mishahara au kufanya mauzo nje ya eneo la CRIZ, basi Fomu ya Ziada ya Mgawanyo wa Kodi (APP) ni lazima ijazwe ili kukokotoa kiasi cha kuripoti kwenye SAFU B (Sehemu ya Eneo lilipo CRIZ).**

| | | |
|---|---|---|
| Imelipwa kwa marejesho ya kodi | $ | 5,000.00 |
| Malipo ya makadirio ya robo mwaka | $ | 60,000.00 |
| Jumla ya Kodi ya Mapato ya Kampuni Iliyolipwa | $ | 65,000.00 |
| Ukizidisha na Asilimia ya Kodi (mfano APP) | | 0.420477 |
| Sehemu ya CRIZ | $ | 27,331.01 |

**Jumla ya Malipo ya Kodi Yaliyofanywa**

**Maeneo Yote Yaliyopo Pennsylvania (Safu A)**

$ 65,000.00 Jumla ya kodi iliyotumwa kwa njia ya malipo, iliyopokelewa na idara ili kuunganishwa na kodi halisi ya mapato ya kampuni.

**Mahali pa CRIZ (Safu B)**

$ 27,331.01 Jumla ya Kodi Halisi ya Mapato ya Kampuni Iliyohusishwa na eneo ndani ya CRIZ.

**Jumla ya Marejesho ya Kodi Yaliyopokelewa**

**Maeneo Yote Yaliyopo Pennsylvania (Safu A)**

$ 0 Marejesho yaliyotolewa kwa Kodi Halisi ya Mapato ya Kampuni.

**Mahali pa CRIZ (Safu B)**

$ 0 Marejesho yaliyotolewa, yanayohusishwa na eneo lililopo ndani ya CRIZ kwa kodi halisi ya mapato ya kampuni.

**Kipengele cha Ugawaji wa Malipo ya Kodi**

Tafadhali toa asilimia ya kodi halisi ya mapato inayohusishwa na eneo lililopo ndani ya CRIZ:

42.05 %.

Mfano
BNK

# Kodi ya Hisa za Benki Mwaka 2025

## Mfano Company, Inc.

## Kodi ya Hisa za Benki Iliyolipwa Kuanzia 1/1/2025 hadi 12/31/2025

Mfano Company, Inc. inamiliki benki mbili ndani ya Pennsylvania ambazo zinatozwa kodi ya hisa za benki; benki moja ipo kwenye eneo la CRIZ. Mnamo Machi 2025 walikamilisha PA RCT-132 (Ripoti ya Kodi ya Hisa na Kodi ya Mkopo).
Kodi iliyostahili kulipwa ilifikia kiasi cha $25,000 na ililipwa wakati wa kuwasilisha ripoti.

***KUMBUKA: Ripoti hii imeandaliwa kwa kuzingatia pesa taslimu iliyolipwa. Kiasi kinaripotiwa katika kipindi ambacho kinalipwa, sio wakati kinapotakiwa kulipwa.***

**KUMBUKA: Kama kampuni ipo ndani ya CRIZ lakini ina tawi eneo lingine, au ina mali, inatoa mishahara au kufanya mauzo nje ya eneo la CRIZ, basi Fomu ya Ziada ya Mgawanyo wa Kodi (APP) ni lazima ijazwe ili kukokotoa kiasi cha kuripoti kwenye SAFU B (Sehemu ya Eneo lilipo CRIZ).**

| | | |
|---|---|---|
| Kodi Iliyolipwa | $ | 25,000.00 |
| Ikizidishwa na Asilimia ya Kodi (mfano APP) | | 0.420477 |
| Sehemu ya CRIZ | $ | 10,511.93 |

**Jumla ya Malipo ya Kodi Yaliyofanywa**

**Maeneo Yote ya Pennsylvania (Safu A)**
$ 25,000.00 Jumla ya kodi iliyotumwa kwa njia ya malipo, iliyopokelewa na idara ili kuunganishwa na kodi iliyotambuliwa juu.

**Mahali pa CRIZ (Safu B)**
$ 10,511.93 Jumla ya aina ya kodi iliyotambuliwa hapo juu na kuhusishwa na eneo lililo ndani ya CRIZ.

**Jumla ya Marejesho ya Kodi Yaliyopokelewa**

**Maeneo Yote ya Pennsylvania (Safu A)**
$ 0 Marejesho yaliyotolewa kwa aina ya kodi jumuishi iliyobainishwa hapo juu.

**Mahali pa CRIZ (Safu B)**
$ 0 Marejesho yanatolewa kwa aina ya kodi iliyotambuliwa hapo juu inayohusishwa na eneo lilipo ndani ya eneo la CRIZ.

**Kipengele cha Ugawaji wa Malipo ya Kodi**

Tafadhali toa asilimia ya aina ya kodi iliyotambuliwa hapo juu inayohusishwa na eneo lililopo ndani ya eneo la CRIZ:
42.05 %.

# Kodi ya Malipo ya Bima Mwaka 2025

## Mfano Company, Inc.

## Kodi Iliyolipwa kuanzia 1/1/2025 hadi 12/31/2025

Mfano IPT

Mfano Company, Inc. inamiliki makampuni mawili ya bima ndani ya Pennsylvania; kampuni moja ipo eneo la CRIZ. Kampuni ililipa kodi ya malipo, jumla ya $20,000 mwaka 2015.

***KUMBUKA: Ripoti hii imeandaliwa kwa kuzingatia pesa taslimu iliyolipwa. Kiasi kinaripotiwa katika kipindi ambacho kinalipwa, sio wakati kinapotakiwa kulipwa.***

**KUMBUKA: Kama kampuni ipo ndani ya CRIZ lakini ina tawi eneo lingine, au ina mali, inatoa mishahara au kufanya mauzo nje ya eneo la CRIZ, basi Fomu ya Ziada ya Mgawanyo wa Kodi (APP) ni lazima ijazwe ili kukokotoa kiasi cha kuripoti kwenye SAFU B (Sehemu ya Eneo lilipo CRIZ).**

| | | |
|---|---|---|
| Kodi Iliyolipwa | $ | 20,000.00 |
| Ukizidisha na Asilimia ya Kodi (mfano APP) | | 0.420477 |
| Sehemu ya CRIZ | $ | 8,409.54 |

**Jumla ya Malipo ya Kodi Yaliyofanywa**

**Maeneo Yote ya Pennsylvania (Safu A)**

$ 20,000.00 Jumla ya kodi iliyotumwa kwa njia ya malipo, iliyopokelewa na idara ili kuunganishwa na kodi iliyotambuliwa juu.

**Mahali pa CRIZ (Safu B)**

$ 8,409.54 Jumla ya aina ya kodi iliyotambuliwa hapo juu na kuhusishwa na eneo lililo ndani ya CRIZ.

**Jumla ya Marejesho ya Kodi Yaliyopokelewa**

**Maeneo Yote ya Pennsylvania (Safu A)**

$ 0 Marejesho yaliyotolewa kwa aina ya kodi jumuishi iliyobainishwa hapo juu.

**Mahali pa CRIZ (Safu B)**

$ 0 Marejesho yanatolewa kwa aina ya kodi iliyotambuliwa hapo juu inayohusishwa na eneo lilipo ndani ya eneo la CRIZ.

**Kipengele cha Ugawaji wa Malipo ya Kodi**

Tafadhali toa asilimia ya aina ya kodi iliyotambuliwa hapo juu inayohusishwa na eneo lililopo ndani ya eneo la CRIZ:

42.05 %.

Mfano
SU

# Ratiba ya Malipo ya Kodi Halisi ya Mauzo ya PA, Matumizi na Makazi ya Hotelini ya Mwaka 2025

## Mfano Company, Inc.

## Kodi ya Mauzo na Matumizi Iliyolipwa Kuanzia 1/1/2025 hadi 12/31/2025

Mfano Company, Inc. ina maduka mawili; moja lipo ndani ya eneo la CRIZ na lingine lipo Harrisburg. Kwenye duka lililopo eneo la CRIZ kwa mwaka walikuwa na mauzo ya $2,000,000 na kwenye duka la Harrisburg walikuwa na mauzo ya $4,000,000, hivyo kuwa na jumla ya mauzo ya $6,000,000.

Mwaka 2025 kampuni ililipa kodi ya mauzo na matumizi kwa Idara ya Mapato ya PA, kwa kutumia Fomu ya PA-3 (Marejesho ya Kodi ya Mauzo, Matumizi na Makazi ya Hotelini) au kupitia myPath, mnamo Januari, Aprili na Oktoba ambayo ilifikia jumla ya $360,000 kwa mwaka. Mnamo Februari mwaka 2025, walipokea marejesho ya kiasi cha $250 kwa malipo ya ziada waliyofanya ya kodi ya mauzo kwenye robo ya 4 ya mwaka 2024.

***KUMBUKA: Ripoti hii imeandaliwa kwa kuzingatia pesa taslimu iliyolipwa. Kiasi kinaripotiwa katika kipindi ambacho kinalipwa, sio wakati kinapotakiwa kulipwa.***

| | Mauzo ya Duka | Manunuzi Yanakatwa Kodi ya Manunuzi ya @ 6% | Kodi ya Mauzo/Matumizi Iliyotumwa @6% | Marejesho |
|---|---|---|---|---|
| Jumla ya Kodi ya Mauzo | $ 6,000,000.00 | - | $ 360,000.00 | $ 250.00 |
| Sehemu ya CRIZ Iliyolipwa Ushuru | $ 2,000,000.00 | - | $ 120,000.00 | $ 83.00 |

**Jumla ya Malipo ya Kodi Yaliyofanywa**

**Maeneo Yote ya Pennsylvania (Safu A)**

$ 360,000.00 Jumla ya kodi iliyotumwa kwa njia ya malipo, iliyopokelewa na idara kwa mauzo yaliyounganishwa, matumizi na makazi ya hotelini

**Mahali pa CRIZ (Safu B)**

$ 120,000.00 Jumla ya kodi ya mauzo, matumizi na makazi ya hotelini inayohusishwa na eneo la ndani ya CRIZ.

**Jumla ya Marejesho ya Kodi Yaliyopokelewa**

**Maeneo Yote ya Pennsylvania (Safu A)**

$ 250.00 Marejesho yaliyotolewa kwenye akaunti ya jumla ya mauzo, matumizi na makazi ya hotelini.

**Mahali pa CRIZ (Safu B)**

$ 83.00 Marejesho yaliyotolewa yanayohusishwa na eneo ndani ya CRIZ kwa kodi za mauzo, matumizi na makazi ya hotelini.

# Ratiba ya Kodi ya Mauzo, Matumizi na Makazi ya Hoteli ya PA kwa Mwaka 2025

**Mfano Company, Inc.**

**Kodi ya Makazi ya Hoteli Iliyolipwa Kuanzia 1/1/2025 hadi 12/31/2025**

Mfano HO

Mfano Company, Inc., inasimamia uendeshaji wa hoteli na pia inamiliki hoteli kadhaa zilizopo maeneo mbalimbali ya Pennsylvania.
Kampuni hii ina hoteli moja ambayo ipo ndani ya eneo la CRIZ. Mwaka 2025 kampuni hii ililipa kiasi cha $60,000 kama kodi ya makazi ya hoteli kwa Idara ya Mapato ya PA, kwa kutumia fomu ya PA-3 (Marejesho ya Kodi ya Mauzo, Matumizi na Makazi ya Hotelini) au kupitia myPath ambayo kati ya kiasi hicho $20,000 ilikuwa inahusiana na eneo la CRIZ.

***KUMBUKA: Ripoti hii imeandaliwa kwa kuzingatia pesa taslimu iliyolipwa. Kiasi kinaripotiwa katika kipindi ambacho kinalipwa, sio wakati kinapotakiwa kulipwa.***

| | Kiasi cha Makazi ya Hoteli Kilichotumwa @6% |
|---|---|
| Jumla ya Kodi ya Makazi ya Hoteli Iliyolipwa | $ 60,000.00 |
| Jumla ya Kodi ya Makazi ya Hoteli Iliyolipwa – Eneo lililopo CRIZ | $ 20,000.00 |

**Jumla ya Malipo ya Kodi Yaliyofanywa**

**Maeneo Yote ya Pennsylvania (Safu A)**

$ 60,000.00 Jumla ya kodi iliyotumwa kwa njia ya malipo, iliyopokelewa na idara kwa mauzo yaliyounganishwa, matumizi na makazi ya hotelini

**Mahali pa CRIZ (Safu B)**

$ 20,000.00 Jumla ya kodi ya mauzo, matumizi na makazi ya hotelini inayohusishwa na eneo la ndani ya CRIZ.

**Jumla ya Marejesho ya Kodi Yaliyopokelewa**

**Maeneo Yote ya Pennsylvania (Safu A)**

$ 0 Marejesho yaliyotolewa kwenye akaunti ya kodi ya jumla ya mauzo, matumizi na makazi ya hotelini.

**Mahali pa CRIZ (Safu B)**

$ 0 Marejesho yaliyotolewa yanayohusishwa na eneo ndani ya CRIZ kwa kodi za mauzo, matumizi na makazi ya hotelini.

## Ratiba ya Kodi ya Zuio la Mwajiri ya PA kwa Mwaka 2025

### Mfano Company, Inc.

### Kodi za Mshahara zilizolipwa Kuanzia 1/1/2025 hadi 12/31/2025

Mfano EWH

Mfano Company, Inc. ina ofisi mbili; moja ipo ndani ya eneo la CRIZ na nyingine ipo Harrisburg. Wana wafanyakazi wanne, wawili wanafanya kazi kwenye ofisi iliyopo ndani ya eneo la CRIZ. Mwaka 2025 kampuni hii ililipa kodi ya zuio kwa Idara ya Mapato ya PA kwa kutumia Fomu ya PA-W3 (Rejesho la Robo ya Mwaka la Kodi ya Zuio la Mwajiri), mnamo Januari (Q4-2024), Aprili (Q1-2025), Julai (Q2-2025) na Oktoba (Q3-2025) ambapo jumla yake ilikuwa ni $3,714.70 kwa mwaka.

***KUMBUKA: Ripoti hii imeandaliwa kwa kuzingatia pesa taslimu iliyolipwa. Kiasi kinaripotiwa katika kipindi ambacho kinalipwa, sio wakati kinapotakiwa kulipwa.***

| | Walioajiriwa kwenye ofisi ya eneo la CRIZ | Jumla ya Mishahara Kabla ya Makato | Zuio la Jimbo @ 3.07% | |
|---|---|---|---|---|
| Mfanyakazi wa #1 | Ndiyo | $ 42,000.00 | $ 1,289.40 | $2,333.20 |
| Mfanyakazi wa #2 | Ndiyo | $ 34,000.00 | $ 1,043.80 | |
| Mfanyakazi wa #3 | Hapana | $ 30,000.00 | $ 921.00 | |
| Mfanyakazi wa #4 | Hapana | $ 15,000.00 | $ 460.50 | |
| | | $ 121,000.00 | $ 3,714.70 | |

**Jumla ya Malipo ya Kodi Yaliyofanywa**

**Maeneo Yote ya Pennsylvania (Safu A)**

$ 3,714.70 Jumla ya kodi iliyotumwa kwa njia ya malipo, iliyopokelewa na idara kwa jumuisho la zuio la mwajiri

**Mahali pa CRIZ (Safu B)**

$ 2,333.20 Jumla ya kiasi cha zuio la mwajiri kinachohusishwa na eneo lililopo ndani ya CRIZ.

**Jumla ya Marejesho ya Kodi Yaliyopokelewa**

**Maeneo Yote ya Pennsylvania (Safu A)**

$ 0 Marejesho yaliyotolewa kwa Akaunti ya Zuio ya Mwajiri Jumuishi.

**Mahali pa CRIZ (Safu B)**

$ 0 Marejesho yaliyotolewa yanayohusishwa na eneo ndani ya CRIZ kwa mwajiri.

## Impuesto Kodi ya Zuio la Mwajiri ya PA – Mradi wa CRIZ 2025
### Mfano Company, Inc.
### Kodi za Mshahara Zilizolipwa kuanzia 1/1/2025 hadi 12/31/2025

Mfano
Mradi wa EWH-CRIZ

**TAFADHALI JAZA RIPOTI YA CRIZ TOFAUTI (YENYE NAMBA YA KIPEKEE YA ENEO) KWA KILA ANUANI YA MRADI WA CRIZ**

Mfano Company, Inc. inafanya kazi kwenye mradi wa CRIZ kama mkandarasi. Ina watu wawili wanaofanya kazi kwenye mradi huo. Kila mtu anayefanya kazi kwenye mradi anatumia asilimia tofauti ya masaa yake ya kazi kwenye mradi. Kodi zilizolipwa zinazohusiana na masaa waliyofanya kazi kwenye mradi ambazo zilitumwa kwenye Idara ya Mapato ya PA, kwa kutumia Fomu ya PA-W3 (Rejesho la Robo ya Mwaka la Kodi ya Zuio la Mwajiri), mnamo Januari (Q4-2024), Aprili (Q1-2025), Julai (Q2-2025) na Oktoba (Q3-2025) ambapo jumla yake ilikuwa ni $805.88 kwa mwaka

| | Kufanya kazi kwenye mradi wa CRIZ | Jumla ya Mishahara Kabla ya Makato | Zuio @ 3.07% | Asilimia ya jumla ya muda liotumika kufanya azi kwenye Mradi a CRIZ | Jumla ya Mishahara Kabla ya Makato inayohusiana na Mradi wa CRIZ | Zuio @ 3.07% |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mfanyakazi wa #1 | Hapana | $ 42,000.00 | $ 1,289.40 | 0% | $ - | $ - |
| Mfanyakazi wa #2 | Hapana | $ 34,000.00 | $ 1,043.80 | 0% | $ - | $ - |
| Mfanyakazi wa #3 | Ndiyo | $ 30,000.00 | $ 921.00 | 65% | $ 19,500.00 | $ 598.65 |
| Mfanyakazi wa #4 | Ndiyo | $ 15,000.00 | 460.50 | 45% | $ 6,750.00 | $ 207.23 |
| | | $ 121,000.00 | $ 3,714.70 | | $ 26,250.00 | $ 805.88 |

**Jumla ya Malipo ya Kodi Yaliyofanywa**

**Maeneo Yote Yaliyopo Pennsylvania (Safu A)**

$ 3,714.70 Jumla ya kodi iliyotumwa kwa njia ya malipo, iliyopokelewa na idara kwa jumuisho la zuio la mwajiri.

**Mahali pa CRIZ (Safu B)**

$ 805.88 Jumla ya kiasi cha zuio la mwajiri kinachohusishwa na mradi wa CRIZ

**Jumla ya Marejesho ya Kodi Yaliyopokelewa**

**Maeneo Yote Yaliyopo Pennsylvania (Safu A)**

$ 0 Marejesho yaliyotolewa yanayohusishwa na jumla ya zuio la mwajiri.

**Mahali pa CRIZ (Safu B)**

$ 0 Marejesho yaliyotolewa yanayohusishwa na Mradi wa CRIZ.

## Kodi ya Kinywaji cha Bia – Ni Lazima Kuwa na Namba ya Akaunti ya Kinywaji cha Bia 2025

**Mfano Company, Inc.**

**Kodi Iliyolipwa kuanzia 1/1/2025 hadi 12/31/2025**

Mfano
MALT

Mfano Company, Inc. inamiliki viwanda vya kutengeneza bia ndani ya Pennsylvania; kimoja kipo ndani ya CRIZ. Mnamo 2025 kampuni iliwasilisha Fomu ya REV-1052 (Ripoti ya Kila Mwezi ya Mtengenezaji na Muagizaji Mwenye Dhamana wa PA ya Bia Inayotakiwa kulipiwa Kodi Inayouzwa kwa Wasambazaji au Wateja au Vyote Pamoja kwa ajili ya Kuuzwa Tena ndani ya PA) kila mwezi na kulipa jumla ya $3,100 kama kodi kwa mwaka (ni lazima kuwa na Namba ya Akaunti ya Kinywaji cha Bia).

***KUMBUKA: Ripoti hii imeandaliwa kwa kuzingatia pesa taslimu iliyolipwa. Kiasi kinaripotiwa katika kipindi ambacho kinalipwa, sio wakati kinapotakiwa kulipwa.***

| | | |
|---|---|---|
| Kodi Iliyolipwa | $ | 3,100.00 |
| Sehemu ya CRIZ | $ | 1,303.00 |

**Jumla ya Malipo ya Kodi Yaliyofanywa**

**Maeneo Yote ya Pennsylvania (Safu A)**

$ 3,100.00 Jumla ya kodi iliyotumwa kwa njia ya malipo, iliyopokelewa na idara ili kuunganishwa na kodi iliyotambuliwa juu.

**Mahali pa CRIZ (Safu B)**

$ 1,303.00 Jumla ya aina ya kodi iliyotambuliwa hapo juu na kuhusishwa na eneo lililo ndani ya CRIZ.

**Jumla ya Marejesho ya Kodi Yaliyopokelewa**

**Maeneo Yote ya Pennsylvania (Safu A)**

$ 0 Marejesho yaliyotolewa kwa aina ya kodi jumuishi iliyobainishwa hapo juu.

**Mahali pa CRIZ (Safu B)**

$ 0 Marejesho yanayotolewa kwa aina ya kodi iliyotambuliwa hapo juu inayohusishwa na eneo lilipo ndani ya eneo la CRIZ.

**ImpKodi za Mauzo na Matumizi kwa manunuzi ya vifaa vinavyotumika kwenye ujenzi ndani ya CRIZ (Mradi wa CRIZ) 2025**
**Mfano Company, Inc.**
**Kodi za Mauzo na Manunuzi zilizolipwa kuanzia 1/1/2025 hadi 12/31/2025**

Mfano
C-SU

***KUMBUKA: Mlipa kodi ni lazima awe na ushahidi wa ankara ili kuthibitisha kiasi kilichoripotiwa na kuwa na Tarehe ya Ankara, Namba ya Ankara, Kiasi cha Manunuzi, na Kodi Iliyolipwa vilivyopo kwa ajili ya kuweka muda wa kuwasilisha.***

| Tarehe ya Ankara | Namba ya Ankara | Kiasi cha Manunuzi | Kodi ya Mauzo Iliyolipwa | Muuzaji aliyetajwa kwenye Ankara |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| 2/15/25 | 12568 | $1,700,000.00 | $102,000.00 | |
| 3/7/25 | 1257 | $750,000.00 | $45,000.00 | |
| 4/15/25 | 18825 | $125.00 | $7.50 | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| Jumla | | $2,450,125.00 | | |
| | | | | |
| Mradi wa CRIZ | | JUMLA | **$147,007.50** | |

***KUMBUKA: Hapo juu panapaswa kujumuisha jumla ya malipo ya kodi ya mauzo ya ankara kwenda kwa muuzaji au msambazaji na/au malipo kwa Pennsylvania kwa kodi ya matumizi ya ankara zisizotoza kodi ya mauzo.**

**KUMBUKA - Safu A na B ni sawa kwa kuwa hii ni kodi iliyolipwa kwa Mradi wa CRIZ (kila Mradi wa CRIZ ni lazima uwasilishe ripoti yake wenyewe kwa kutumia Anuani ya Mradi wa CRIZ iliyoidhinishwa).**

## Jumla ya Malipo ya Kodi Yaliyofanywa

**Maeneo Yote ya Pennsylvania (Safu A)**

$ 147,007.50 Jumla ya kodi iliyotumwa kwa njia ya malipo, iliyopokelewa na idara ili kuunganishwa na kodi iliyotambuliwa juu.

**Mradi wa CRIZ (Safu B)**

$ 147,007.50 Jumla ya aina ya kodi iliyotambuliwa hapo juu na kuhusishwa na eneo lililo ndani ya CRIZ.

## Jumla ya Marejesho ya Kodi Yaliyopokelewa

**Maeneo Yote ya Pennsylvania (Safu A)**

$ 0 Marejesho yaliyotolewa kwa aina ya kodi jumuishi iliyobainishwa hapo juu.

**Mradi wa CRIZ (Safu B)**

$ 0 Marejesho yanatolewa kwa aina ya kodi iliyotambuliwa hapo juu inayohusishwa na eneo lilipo ndani ya eneo la CRIZ.

**Mfano TPP**

# Kodi za Mauzo au Manunuzi yaliyofanyika PA ya Mali Binafsi Zinazoshikika au Huduma 2025

## Mfano Company, Inc.

### Kodi za Mauzo na Manunuzi Zilizolipwa kuanzia 1/1/2025 hadi 12/31/2025

Mfano Company, Inc. ina maduka mawili; moja lipo ndani ya eneo la CRIZ na lingine lipo Harrisburg. Kampuni hiyo ilinunua samani na mali zingine binafsi zinazoshikika zenye jumla ya thamani ya $150,000 ambapo kiasi cha $75,000 kilikuwa ni kwa eneo lililokuwa kwenye CRIZ.

***KUMBUKA: Ripoti hii imeandaliwa kwa kuzingatia pesa taslimu iliyolipwa. Kiasi kinaripotiwa katika kipindi ambacho kinalipwa, sio wakati kinapotakiwa kulipwa.***

| | **Safu A** | | **Safu B** |
|---|---|---|---|
| TPP au Huduma Zilizonunuliwa Jumla PA | Jumla ya Mauzo ya TPP ya PA au Kodi ya Matumizi @ 6% | TPP au Huduma Zilizonunuliwa Ndani ya CRIZ | Jumla ya Mauzo ya TPP ya CRIZ au Kodi ya Matumizi @ 6% |
| $ 150,000.00 | $ 9,000.00 | $ 75,000.00 | $ 4,500.00 |

***KUMBUKA: Mlipa kodi ni lazima awe na ushahidi wa kiasi kilichoripotiwa na kuwa na Tarehe ya Ankara, Namba ya Ankara, Kiasi cha Manunuzi, na Kodi Iliyolipwa vilivyopo kwa ajili ya kuweka muda wa kuwasilisha.***

**Jumla ya Malipo ya Kodi Yaliyofanywa**

**Maeneo Yote ya Pennsylvania (Safu A)**

$ 9,000.00 Jumla ya kodi iliyotumwa kwa njia ya malipo, iliyopokelewa na idara kwa ajili ya mauzo au kodi ya matumizi ya huduma au mali binafsi zinazoshikika zilizonunuliwa.

**Mahali pa CRIZ (Safu B)**

$ 4,500.00 Jumla ya mauzo au kodi ya matumizi iliyolipwa kwa manunuzi ya mali binafsi zinazoshikika au huduma iliyotumiwa na biashara tu kwa ajili ya shughuli zinazofanyika ndani ya eneo (eneo la CRIZ).

**Jumla ya Marejesho ya Kodi Yaliyopokelewa**

**Maeneo Yote ya Pennsylvania (Safu A)**

$ 0 Marejesho yaliyotolewa yanayohusishwa na maeneo yote ndani ya PA.

**Mahali pa CRIZ (Safu B)**

$ 0 Marejesho yaliyotolewa yanayohusishwa na eneo ndani ya CRIZ.

**Kodi ya Mapato Binafsi (PIT) Inayokatwa kwenye Mapato Yaliyopita Kwenye Biashara 2025**
**Mfano Company, Inc.**
**Kodi Iliyolipwa kuanzia 1/1/2025 hadi 12/31/2025**

Mfano
PIT

Mfano Company, Inc. ni Kampuni Inayopitisha Tu Iliyopo Pennsylvania yenye mmiliki mmoja wa hisa. Kwa mwaka 2024, kampuni hiyo iliripoti mapato halisi ya $500,000. Hakuna kodi ya zuio la kipato kwa PA iliripotiwa na kampuni. Mnamo Machi 2025 mmiliki wa hisa alilipa $15,350 kama kodi ya kipato binafsi ndani ya Pennsylvania kwa Mamlaka ya Idara ya Mapato ya PA kwa kipato hiki kiwango cha 3.07%

Makampuni ya kupitisha tu ni pamoja na
- -Mmiliki mmoja
- -S Corporation
- -LLC
- -Ushirika
- -LP (Ushirika wa Makampuni)

***KUMBUKA: Ripoti hii imeandaliwa kwa kuzingatia pesa taslimu iliyolipwa. Kiasi kinaripotiwa katika kipindi ambacho kinalipwa, sio wakati kinapotakiwa kulipwa.***

**KUMBUKA: HAIHUSISHI PIT kwenye kipato kisichohusisha Utendaji wa Moja kwa Moja**

| | | |
|---|---|---|
| Impuestos pagados | $ | 15,350.00 |
| Parte CRIZ | $ | 15,350.00 |

## Jumla ya Malipo ya Kodi Yaliyofanywa

### Maeneo Yote ya Pennsylvania (Safu A)

$ 15,350.00 Jumla ya kodi iliyotumwa kwa njia ya malipo, iliyopokelewa na idara ili kuunganishwa na kodi iliyotambuliwa juu.

### Mahali pa CRIZ (Safu B)

$ 15,350.00 Jumla ya aina ya kodi iliyotambuliwa hapo juu na kuhusishwa na eneo lililo ndani ya CRIZ.

## Jumla ya Marejesho ya Kodi Yaliyopokelewa

### Maeneo Yote ya Pennsylvania (Safu A)

$ 0 Marejesho yaliyotolewa kwa aina ya kodi jumuishi iliyobainishwa hapo juu.

### Mahali pa CRIZ (Safu B)

$ 0 Marejesho yanatolewa kwa aina ya kodi iliyotambuliwa hapo juu inayohusishwa na eneo lilipo ndani ya eneo la CRIZ.

**Kodi ya Bia au Vinywaji Vilivyochachushwa –**
**Kodi ya Ushuru na Kodi ya Mauzo**
**2025**
**Mfano Company, Inc.**
**Kodi Iliyolipwa kuanzia 1/1/2025 hadi 12/31/2025**

Mfano
MALT
EX+SLS

Mfano Company, Inc. inamiliki migahawa miwili ndani ya Pennsylvania; mmoja upo ndani ya eneo la CRIZ. Mnamo mwaka 2025 kampuni ilinunua mapipa 462 ya bia kwa gharama ya $65,604.25; mapipa 275 yalikuwa kwenye eneo la CRIZ kwa gharama ya $39,050.25.

***KUMBUKA: Ripoti hii imeandaliwa kwa kuzingatia pesa taslimu iliyolipwa. Kiasi kinaripotiwa katika kipindi ambacho kinalipwa, sio wakati kinapotakiwa kulipwa.***

***KUMBUKA: Mlipa kodi ni lazima awe na ushahidi wa ankara mbalimbali za kuthibitisha kiasi kilichoripotiwa na kuwa na Tarehe ya Ankara, Namba ya Ankara, Kiasi cha Manunuzi, na Kodi Iliyolipwa vilivyopo kwa ajili ya kuweka muda wa kuwasilisha.***

Kumbuka - Tazama Kodi ya Ushuru na Viwango vya Kodi hapo chini

**Ushuru wa Malt au Kinywaji cha Bia na Kodi ya Mauzo**

| | CRIZ |
|---|---|
| | 275 |
| Jumla ya gharama ya Malt au Vinywaji Vilivyotengenezwa Vilivyonunuliwa kwa ajili ya kuuzwa tena katika eneo hilo | $ 2.48 |
| | $ 682.00 |
| Kodi ya Mauzo Iliyolipwa (6%) | |
| Jumla ya gharama ya Malt au Vinywaji vya Bia | $ 39,050.25 |
| vilivyonunuliwa kwa ajili ya kuuzwa tena kwenye eneo la mpango | $ 2,343.02 |

**Aina ya Kodi:** **Kodi ya Ushuru ya Malt au Kinywaji cha Bia**

**Ujazo Ulionunuliwa kwa ajili ya kuuzwa tena kwenye eneo la mpango**
275 Mapipa

**Kodi ya Ushuru iliyolipwa kwa eneo la CRIZ**
$ 682.00 Jumla ya aina ya kodi iliyotambuliwa hapo juu na kuhusishwa na eneo lililo ndani ya CRIZ.

| Viwango vya Kodi ya Ushuru wa Malt au Kinywaji cha Bia (kwa ujazo wake) | |
|---|---|
| Pipa 1 | $ 2.48 |
| Pipa 1/2 | $ 1.24 |
| Lita 50 | $ 1.06 |
| Galoni 12 | $ 0.96 |
| Pipa 1/4 | $ 0.62 |
| Pipa 1/6 | $ 0.42 |
| Pipa 1/8 | $ 0.32 |
| Aunsi 160 | $ 0.10 |
| Lita 4 | $ 0.09 |
| Galoni 12 | $ 0.08 |
| Lita 2 | $ 0.05 |
| Aunsi 40 | $ 0.03 |
| Kwati 1 | $ 0.02 |
| Aunsi 25 | $ 0.02 |
| Painti 1 | $ 0.01 |
| Painti 1/2 | $ 0.0066 |

**Aina ya Kodi:** **Kodi ya Mauzo ya Malt au Kinywaji cha Bia**

**Jumla ya gharama ya malt au vinywaji vya bia vilivyonunuliwa kwa ajili ya kuuzwa tena kwenye eneo la mpango**
$ 39,050.25

**Kodi ya mauzo iliyolipwa kwa malt au vinywaji vya bia vilivyonunuliwa kwa ajili ya kuuzwa tena kwenye eneo la mpango (eneo la CRIZ)**
$ 2,343.02 Jumla ya aina ya kodi iliyotambuliwa hapo juu na kuhusishwa na eneo lililo ndani ya CRIZ.

## Ushuru wa Pombe Kali/Mvinyo na Kodi ya Mauzo 2025

**.Mfano Company, Inc**

**Kodi Iliyolipwa kuanzia 1/1/2025 hadi 12/31/2025**

Mfano
LIQR

Mfano Company, Inc. inamiliki migahawa miwili ndani ya Pennsylvania; mmoja upo ndani ya eneo la CRIZ. Mnamo mwaka 2025 kampuni ilinunua pombe kali/mvinyo wa thamani ya $50,000 kutoka mapipa 462 ya bia kwa gharama ya $65,604.25; mapipa 275 yalikuwa kwenye eneo la CRIZ kwa gharama ya $39,050.25

***KUMBUKA: Ripoti hii imeandaliwa kwa kuzingatia pesa taslimu iliyolipwa. Kiasi kinaripotiwa katika kipindi ambacho kinalipwa, sio wakati kinapotakiwa kulipwa.***

***KUMBUKA: Mlipa kodi ni lazima awe na ushahidi wa ankara mbalimbali za kuthibitisha kiasi kilichoripotiwa na kuwa na Tarehe ya Ankara, Namba ya Ankara, Kiasi cha Manunuzi, na Kodi Iliyolipwa vilivyopo kwa ajili ya kuweka muda wa kuwasilisha***

**Jumla ya kodi iliyohusishwa na Pombe Kali/Mvinyo ulionunuliwa ili Kuuzwa tena kwenye Eneo la Mpango (Ushuru na Kodi ya Mauzo)**

| | | |
|---|---|---|
| Jumla ya gharama ya pombe kali na/au mvinyo ulionunuliwa kwa ajili ya kuuzwa tena kwenye eneo la mpango | $ | 40,000.00 |
| Kodi ya Ushuru wa Pombe Kali/Mvinyo (14.39%) iliyoambatanishwa kwenye bei ya manunuzi | $ | 5,756.00 |
| Kodi ya Mauzo ya Pombe Kali/Mvinyo Iliyolipwa (5.66% ya bei ya manunuzi) | $ | 2,264.00 |
| Jumla ya kodi iliyohusishwa na pombe kali na/au mvinyo ulionunuliwa kwa ajili ya kuuzwa tena kwenye eneo la mpango (Ushuru jumlisha na Kodi ya Mauzo) | $ | 8,020.00 |

**Jumla ya gharama za pombe kali na/au mvinyo ulionunuliwa kwa ajili ya kuuzwa tena kwenye eneo la mpango**

$ 40,000.00 Jumla ya kodi iliyotumwa kwa njia ya malipo, iliyopokelewa na idara ili kuunganishwa na kodi iliyotambuliwa juu.

**Kodi ya Ushuru wa Pombe Kali/Mvinyo**

$ 5,756.00 Jumla ya aina ya kodi iliyotambuliwa hapo juu na kuhusishwa na eneo lililo ndani ya CRIZ.

**Kodi ya Mauzo ya Pombe Kali/Mvinyo**

$ 2,264.00 Jumla ya aina ya kodi iliyotambuliwa hapo juu na kuhusishwa na eneo lililo ndani ya CRIZ.

**Jumla ya kodi iliyohusishwa na pombe kali na/au mvinyo ulionunuliwa kwa ajili ya kuuzwa tena kwenye eneo la mpango (eneo la CRIZ) = Ushuru + Kodi ya Mauzo**

$ 8,020.00

Mfano

EIT

# Ratiba ya Mshahara wa Mwajiri Wa Ndani/Kodi ya Kipato Kilichopatikana 2025

**Mfano Company, Inc.**

**Kodi ya Mapato ya Ndani Iliyolipwa kuanzia 1/1/2025 hadi 12/31/2025**

Mfano Company, Inc. ina ofisi katika mji wa Erie iliyopo ndani ya eneo la CRIZ. Wana wafanyakazi wanne; wawili wanaishi katika Jiji la Erie na wengine wawili wanakaa MilcreekTownship. Mwaka 2025 kampuni hii ililipa kodi za zuio kwa wakusanya kodi wa eneo hilo mnamo Januari (Q4-2024), Aprili (Q1-2025), Julai (Q2-2025) na Oktoba (Q3-2025) ambapo jumla yake ilikuwa ni $1,435 kwa mwaka.

***KUMBUKA: Ripoti hii imeandaliwa kwa kuzingatia pesa taslimu iliyolipwa. Kiasi kinaripotiwa katika kipindi ambacho kinalipwa, sio wakati kinapotakiwa kulipwa.***

| | Kuishi Mji wa Erie | Jumla ya Mishahara Kabla ya Makato | Zuio la Eneo Ulipo | |
|---|---|---|---|---|
| Mfanyakazi wa #1 | Ndiyo | $ 42,000.00 | $ 420.00 | **$760.00** |
| Mfanyakazi wa #2 | Ndiyo | $ 34,000.00 | $ 340.00 | |
| Mfanyakazi wa #3 | Hapana | $ 30,000.00 | $ 450.00 | **$675.00** |
| Mfanyakazi wa #4 | Hapana | $ 15,000.00 | $ 225.00 | |
| | | $ 121,000.00 | $ 1,435.00 | |

| AINA YA KODI | Kodi za ndani zilizolipwa na biashara kwa maeneo YOTE ya Jiji la Erie kwa MWAKA WA KALENDA wa 2025 (kupunguza marejesho ya fedha taslimu) | Kodi za ndani zilizolipwa na kuhusishwa na MAENEO YALIYO NDANI YA ERIE kwa MWAKA WA KALENDA wa 2025 (kupunguza marejesho ya fedha taslimu) |
|---|---|---|
| Mshahara wa Mwajiri wa Ndani AU Kodi ya Mapato Yaliyopatikana (EIT) kwa Wafanyakazi au Wamiliki wa Biashara wanaoishi ndani ya Jiji la Erie PEKEE (Wanaoishi PSD 250201) | JUMLA<br>$ 760.00 | JUMLA<br>$ 760.00 |
| Kodi ya Huduma za Ndani (LST) kwa Wafanyakazi au Wamiliki wa Biashara wanaofanya kazi ndani ya Jiji la Erie (Wanaoishi PSD 250201) | JUMLA<br>$ 208.00 | JUMLA<br>$ 208.00 |
| **Jumla ya Kodi zilizotumwa kwa Jiji la Erie zinazohusishwa na BIASHARA ZILIZOPO MAENEO YA CRIZ** | | $ 968.00 |

**Mfano**
**Mradi wa EIT-CRIZ**

# Ratiba ya Mshahara wa Mwajiri Wa Ndani/Kodi ya Kipato Kilichopatikana - Mradi wa CRIZ
## 2025

**Mfano Company, Inc.**

**Kodi ya Mapato ya Ndani Iliyolipwa kuanzia 1/1/2025 hadi 12/31/2025**

Mfano Company, Inc. ina ofisi katika ndani ya Millcreek Township lakini inafanyia kazi Mradi Ulioidhinishwa na Mamlaka wa CRIZ. Wana wafanyakazi wanne; wawili wanaishi katika Jiji la Erie na wengine wawili wanakaa Milcreek Township lakini kati ya wale wanaoishi Erie ni mmoja tu ndiye anayefanya kazi kwenye mradi huo Ulioidhinishwa na Mamlaka wa CRIZ kwa 50% ya muda wake wa kazi. Mwaka 2025 kampuni hii ililipa kodi za zuio kwa wakusanya kodi wa eneo hilo mnamo Januari (Q4-2024), Aprili (Q1-2025), Julai (Q2-2025) na Oktoba (Q3-2025) ambapo jumla yake ilikuwa ni $1,390 kwa mwaka.

***KUMBUKA: Ripoti hii imeandaliwa kwa kuzingatia pesa taslimu iliyolipwa. Kiasi kinaripotiwa katika kipindi ambacho kinalipwa, sio wakati kinapotakiwa kulipwa.***

| | Kuishi Mji wa Erie | Kufanya kazi kwenye Mradi Ulioidhinishwa wa CRIZ | Jumla ya Mishahara Kabla ya Makato | Zuio la Eneo Ulipo | Zuio la Eneo Ulipo kwa Mradi wa CRIZ |
|---|---|---|---|---|---|
| Mfanyakazi wa #1 | Ndiyo | Ndiyo | $ 52,500.00 | $ 525.00 | $ 262.50 |
| Mfanyakazi wa #2 | Ndiyo | Hapana | $ 34,000.00 | $ 340.00 | $ - |
| Mfanyakazi wa #3 | Hapana | Ndiyo | $ 30,000.00 | $ 300.00 | $ - |
| Mfanyakazi wa #4 | Hapana | Hapana | $ 15,000.00 | $ 225.00 | $ - |
| | | | $ 131,500.00 | $ 1,390.00 | $ 262.50 |

| **AINA YA KODI** | **ENEO AU MAENEO YA MRADI ndani ya Mji wa Erie kwa MWAKA WA KALENDA 2025 (kupunguza marejesho ya fedha taslimu)** |
|---|---|
| Kodi ya Mshahara wa Mwajiri wa Ndani AU Kodi ya Mapato Yaliyopatikana (EIT) kwa wale Wafanyakazi au Wamiliki wa Biashara wanaofanya kazi kwenye Mradi Ulioidhinishwa na Mamlaka wa CRIZ Tu NA wanaoishi kwenye Mji wa Erie (Wanaoishi PSD 250201) | JUMLA<br>$ 262.50 |
| Kodi ya Huduma za Ndani (LST) kwa Wafanyakazi au Wamiliki wa Biashara wanaofanya kazi ndani ya Jiji la Erie (Wanaoishi PSD 250201) | JUMLA<br>$ 26.00 |
| **Jumla ya Kodi zilizotumwa kwenye Jiji la Erie zinazohusishwa na MIRADI YA CRIZ ILIYOIDHINISHWA NA MAM-** | $ 288.50 |

Mfano
LST

# Ratiba ya Kodi ya Huduma ya Ndani
# 2025

**Mfano Company, Inc.**

**Kodi ya Huduma za Ndani Iliyolipwa kuanzia 1/1/2025 hadi 12/31/2025**

Mfano Company, Inc. ina ofisi ndani ya Jiji la Erie. Wana wafanyakazi wanne, wote wanafanya kazi katika ofisi iliyopo katika eneo la CRIZ. Mwaka 2025 kampuni hii ililipa Kodi ya Huduma za wa eneo hilo kwa mamlaka za kukusanya kodi za eneo hilo mnamo Januari (Q4-2024), Aprili (Q1-2025), Julai (Q2-2025) na Oktoba (Q3-2025) ambapo jumla yake ilikuwa ni $208 kwa mwaka.

***KUMBUKA: Ripoti hii imeandaliwa kwa kuzingatia pesa taslimu iliyolipwa. Kiasi kinaripotiwa katika kipindi ambacho kinalipwa, sio wakati kinapotakiwa kulipwa.***

| | Walioajiriwa kwenye ofisi ya CRIZ | Jumla ya Mishahara Kabla ya Makato | LST Iliyolipwa |
|---|---|---|---|
| Mfanyakazi wa #1 | Ndiyo | $ 42,000.00 | $ 52.00 |
| Mfanyakazi wa #2 | Ndiyo | $ 34,000.00 | $ 52.00 |
| Mfanyakazi wa #3 | Ndiyo | $ 30,000.00 | $ 52.00 |
| Mfanyakazi wa #4 | Ndiyo | $ 15,000.00 | $ 52.00 |
| | | $ 121,000.00 | $ 208.00 |

$208.00

| AINA YA KODI | Kodi za ndani zilizolipwa na biashara kwa maeneo YOTE ya Jiji la Erie kwa MWAKA WA KALENDA wa 2025 (kupunguza marejesho ya fedha taslimu) | Kodi za mitaa zilizolipwa na zinazohusishwa na CRIZ LOCATION(S) ndani ya Jiji la Erie katika MWAKA WA KALENDA WA 2025 (kuondoa marejesho ya pesa taslimu) |
|---|---|---|
| Mshahara wa Mwajiri wa Ndani AU Kodi ya Mapato Yaliyopatikana (EIT) kwa Wafanyakazi au Wamiliki wa Biashara wanaoishi ndani ya Jiji la Erie PEKEE (Wanaoishi PSD 250201) | JUMLA<br>$ 760.00 | JUMLA<br>$ 760.00 |
| Kodi ya Huduma za Ndani (LST) kwa Wafanyakazi au Wamiliki wa Biashara wanaofanya kazi ndani ya Jiji la Erie (Wanaoishi PSD 250201) | JUMLA<br>$ 208.00 | JUMLA<br>$ 208.00 |
| **Jumla ya Kodi zilizotumwa kwa Jiji la Erie zinazohusishwa na BIASHARA ZILIZOPO MAENEO YA CRIZ** | | $ 968.00 |

Mfano
Mradi wa LSTCRIZ

# Ratiba ya Kodi ya Huduma ya Ndani – Mradi wa CRIZ 2025

**Mfano Company, Inc.**

**Kodi ya Huduma za Ndani Iliyolipwa kuanzia 1/1/2025 hadi 12/31/2025**

Mfano Company, Inc. ina ofisi Millcreek Township. Na wanafanya kazi kwenye mradi Ulioidhinishwa na Mamlaka wa CRIZ. Wana wafanyakazi wanne, ambapo mmoja anafanya kazi kwenye Mradi Ulioidhinishwa na Mamlaka wa CRIZ kwa 50% ya muda wake wa kazi. Mwaka 2025 kampuni hii ililipa Kodi ya Huduma za wa eneo hilo kwa mamlaka za kukusanya kodi za eneo hilo mnamo Januari (Q4-2024), Aprili (Q1-2025), Julai (Q2-2025) na Oktoba (Q3-2025) ambapo jumla yake ilikuwa ni $208 kwa mwaka.

***KUMBUKA: Ripoti hii imeandaliwa kwa kuzingatia pesa taslimu iliyolipwa. Kiasi kinaripotiwa katika kipindi ambacho kinalipwa, sio wakati kinapotakiwa kulipwa.***

| | Kazi kwenye Mradi Ulioidhinishwa wa CRIZ | Jumla ya Mishahara Kabla ya Makato | LST Iliyolipwa | Mradi wa LST CRIZ |
|---|---|---|---|---|
| Mfanyakazi wa #1 | Ndiyo | $ 52,500.00 | $ 52.00 | $ 26.00 |
| Mfanyakazi wa #2 | Hapana | $ 34,000.00 | $ 52.00 | $ - |
| Mfanyakazi wa #3 | Hapana | $ 30,000.00 | $ 52.00 | $ - |
| Mfanyakazi wa #4 | Hapana | $ 15,000.00 | $ 52.00 | $ - |
| | | $ 131,500.00 | $ 208.00 | $ 26.00 |

| AINA YA KODI | ENEO AU MAENEO YA MRADI ndani ya Mji wa Erie kwa MWAKA WA KALENDA 2025 (kupunguza marejesho ya fedha taslimu) |
|---|---|
| Kodi ya Mshahara wa Mwajiri wa Ndani AU Kodi ya Mapato Yaliyopatikana (EIT) kwa Wale Wafanya-kazi au Wamiliki wa Biashara wanaofanya kazi kwenye Mradi Ulioidhinish-wa na Mamlaka wa CRIZ Tu NA wanaoishi kwenye Mji wa Erie (Wanaoishi PSD 250201) | JUMLA<br>$ 262.50 |
| Kodi ya Huduma za Ndani (LST) kwa Wafanyakazi au Wamiliki wa Biashara wanaofanya kazi ndani ya Jiji la Erie (Wanaoishi PSD 250201) | JUMLA<br>$ 26.00 |
| **Jumla ya Kodi zilizotum-wa kwa Jiji la Erie zinazo-husishwa na BIASHARA ZILIZOPO MAENEO YA CRIZ** | $ 288.50 |

# Ratiba ya Kodi ya Burudani
## 2025
### Mfano Company, Inc.
### Kodi ya Huduma za Ndani Iliyolipwa kuanzia 1/1/2025 hadi 12/31/2025

Mfano
AMT

Mfano Company, Inc. ina maeneo mawili ndani ya Erie. Eneo moja lipo ndani ya mpango wa CRIZ, na lingine lipo nje ya CRIZ. Walilipa jumla ya $1,000 kama kodi ya burudani kwa mwaka 2025, ambapo $500 ilikuwa ni kwa eneo la CRIZ.

| | |
|---|---|
| ***Jumla ya kodi ya burudani mwaka 2025 kwa eneo la CRIZ:*** | $ 500.00 |

# Eneo la Uhuishaji na Uboreshaji wa Jiji (CRIZ)

## Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara

F A Q

## 1 CRIZ ni nini?

CRIZ ni Eneo la Uhuishaji na Uboreshaji wa Jiji ambalo liliundwa kupitia Sheria ya Jimbo—Sheria ya 52 ya 2013, (P.L. 270, Namba 52 ya Julai 9, 2013) iliyorekebishwa hivi karibuni na Sheria ya 84 ya 2025 (P.L. 526, Na. 84 ya Julai 13, 2025)—kama chombo cha uhuishaji wa jiji.

## 2 Madhumuni na faida za CRIZ ni nini?

Madhumuni ya CRIZ ni kutengeneza utaratibu wa ufadhili ambao utasaidia ukuaji endelevu wa uchumi maeneo ya mjini ya jiji na vituo vya biashara vya mtaani. Faida za CRIZ ni pamoja na:

- Kusaidia biashara zibaki kuwa na ushindani au kuongeza ushindani.
- Kuongeza thamani ya majengo na mali zilizopo katika jiji kwa kuyatumia tena majengo yanayotumika kwa kiwango kidogo au yaliyo tupu.
- Biashara zinaweza kunufaika kwa njia isiyo ya moja kwa moja kutokana na uboreshaji wa maeneo ya umma katika eneo la mpango linaloboresha usalama wa watembea kwa miguu na kuongeza maegesho
- Biashara za maduka ya rejareja na migahawa zitafaidika kutokana na ongezeko la wageni na wateja wengi kutokana na biashara mpya zilizopo katika eneo la mradi na kuongezeka kwa biashara za ukarimu.
- Biashara zitafaidika kutokana na kuongezeka kwa mvuto wa maeneo ya mjini na katika vituo vya biashara ambapo wakazi wanaweza kuishi, kufanya kazi, kununua na kufurahia vitu vilivyopo jijini.
- Fursa za kufanya maendeleo upya zitaleta fursa za ajira kwa wakazi wa jiji na kuvutia wakazi wapya kutoka sehemu mbalimbali ambao wataongeza idadi ya wateja kwenye biashara.

## 3 Nani anaisimamia CRIZ?

CRIZ inasimamiwa na Mamlaka ya Erie CRIZ, ambayo ni mamlaka huru inayojitegemea Jumuiya ambayo iliyoundwa kusimamia juhudi za uhuishaji kwenye eneo la CRIZ. Inajumuisha Bodi ya Wakurugenzi ambao hufanya maamuzi yote ya kiutawala. Bodi ya CRIZ hukutana kila mwezi. Kwa maelezo zaidi, ikiwa ni pamoja na maelezo kuhusu mikutano, tembelea tovuti ya Mamlaka ya CRIZ hapa: https://eriecriz.org

## 4 CRIZ inafadhiliwaje?

CRIZ inafadhiliwa kwa kutumia kodi maalum zilizochaguliwa za Jimbo na za Eneo Husika zinazohusishwa na CRIZ ambazo hutumwa kwenye mfuko wa CRIZ. Mamlaka ya CRIZ kisha hutenga rasilimali hizi kupitia miongozo yao ya mradi ili kusaidia katika kuwezesha juhudi za maendeleo ya kiuchumi. Kodi zinazohusishwa na CRIZ sio kodi mpya zinazotozwa kwa mmiliki wa mali au biashara. Kodi zinazohusishwa na CRIZ ni kodi ambazo tayari zinalipwa kwa Jumuiya na kwa Jiji ambazo zinarudishwa kwa Mamlaka ya CRIZ ili zitumike kwa dhumuni la kuleta maendeleo ya kiuchumi.

## 5 CRIZ itadumu kwa muda gani? Je, kuna ukomo wa muda wa CRIZ au biashara yangu itakuwa katika CRIZ siku zote?

Sheria ya CRIZ inaruhusu eneo husika la mpango kuwepo kwa muda wa miaka 30, au mpaka pale ambapo dhumuni la kuundwa kwake litakapotimizwa au dhamana zitakapolipwa.

# Eneo la Uhuishaji na Uboreshaji wa Jiji (CRIZ)

## Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara

F A Q

## 6 Kwa nini Erie inahitaji CRIZ?

Erie inahitaji CRIZ ili kutoa maendeleo ya kiuchumi ya jumla na ya kimkakati maeneo ya mijini mwa jiji na kwenye vituo vya biashara vya mitaani kwa njia za uwezeshaji wa kifedha ili kufanikisha ufanyaji wa uhuishaji.

## 7 Je, nitajuaje kama biashara yangu iko katika eneo la CRIZ?

Wasiliana na Brian Polito, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya CRIZ kupitia 814-679-CRIZ (2749) au kupitia barua pepe kwa brian@eriecriz.org. Atakuambia kama uko kwenye eneo la CRIZ. Au, unaweza kuiangalia biashara yako kwenye ramani rasmi ya CRIZ iliyopo kwenye kiungo kifuatacho: https://tinyurl.com/ErieCRIZmap na ubonyeze kwenye ramani ya CRIZ. Unaweza kukuza ukubwa wa ramani ili kuona sehemu fulani vizuri. Sanduku la habari litajitokeza ukisogeza kibonyezeo juu ya jengo.

## 8 Kuwa ndani ya mpango wa CRIZ kutaathirije wafanyakazi wangu?

CRIZ haitaathiri wafanyakazi wako. Mahitaji yoyote ambayo wafanyakazi wako walikuwa nayo kabla ya kuundwa kwa CRIZ hayaathiriwi na CRIZ.

## 9 Je, ninatakiwa kuripoti? Nini kitatokea nisipofanya hivyo?

Ndiyo. Hili ni hitaji la kisheria na lazima likamilishwe kwa usahihi na kwa wakati (kabla au tarehe 15 Juni kila mwaka). Usipofanya hivyo, adhabu, ambayo ni ndogo tu, chini ya 10% ya kodi zote zinazostahiki kwa mamlaka ya kodi katika mwaka wa kalenda uliopita, au $1000, itatolewa na Idara ya Mapato ya Jimbo kwa hiyo tafadhali wasilisha ripoti zako kwa wakati.
Adhabu hii inatozwa na Jumuiya ya Pennsylvania na Mamlaka ya CRIZ haiwezi kuondoa adhabu hii.
Ni jumuiya pekee ndiyo inaweza kuondoa adhabu hiyo na biashara ni lazima iwasilishe ombi la kuomba msamaha moja kwa moja kwa Idara ya Mapato ya PA.

## 10 Kama shirika langu ni shirika lisilo la faida, je, ninatakiwa kuripoti?

Ndiyo. Mashirika yasiyo ya faida yanatakiwa kuwasilisha ripoti pia. Mashirika ya kiserikali tu ndiyo yamesamehewa kuripoti. Mashirika mengine yote yanatakiwa kuripoti.

## 11 Shirika langu likitaka kuzungumza na mtu kuhusu CRIZ. Je, hilo linawezekana?

Inawezekana kabisa. Wasiliana na Brian Polito, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya CRIZ kupitia 814-679-CRIZ (2749) au kupitia barua pepe brian@eriecriz.org au wasiliana na anayehusika na kuhakikisha sheria na taratibu za CRIZ zinafuatwa, Deana Zosky, kupitia 484-951-1289 au kwa barua pepe Eriecrizcompliance@four-score.com na kupanga miadi ya kukutana.

## 12 Kuwa ndani ya CRIZ kuna athari gani kwangu na kwa biashara yangu?

Kuwa biashara iliyo ndani ya CRIZ inamaanisha kwamba biashara zako zitanufaika kutokana na ukuaji wa uchumi wa Jiji kwa namna mbalimbali, kama vile kuongezeka kwa thamani ya majengo, uboreshaji wa mazingira yanayokuzunguka, kuongezeka kwa mauzo kadri maboresho mapya yanavyozidi kufanyika, na kadri uwezo wa kutuma maombi ya kupata ufadhili wa Mamlaka ya Erie CRIZ kwa ajili ya miradi ya ziada unavyozidi kuongezeka.

## 13 Pesa huwa inaenda wapi?

Kiasi kinachoripotiwa kila mwaka hukaguliwa na vyombo vya kukusanya kodi vya jimbo na vya eneo lako kisha kuthibitishwa na vyombo hivyo na kutumwa kwa Mamlaka ya Erie CRIZ ili kuzitumia taarifa hizo kulingana na sheria na miongozo yao ya mradi na mchakato wao wa kutoa idhini.

## 14 Nani anaamua namna inavyotumika?

Mamlaka ya Erie CRIZ ndiyo inayoamua namna ya kutumia pesa hizo lakini inafanya maamuzi hayo kwa kuzingatia vigezo vya mahitaji ya sheria ya CRIZ.
Jumuiya ya Pennsylvania lazima pia iidhinishe matumizi ya fedha za CRIZ kwa kufuata utaratibu wa kupata idhini wa Mamlaka ya Erie CRIZ.

## 15 Je, biashara yangu inaweza kupata ufadhili kupitia CRIZ? Ikiwa ndio, kwa madhumuni gani? Na inachukua muda gani?

Kama biashara yako inataka kufanya mradi wa maendeleo au kuendeleza upya mradi fulani katika eneo la Erie CRIZ, tafadhali wasiliana na Brian Polito, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya CRIZ kupitia 814-679-CRIZ (2749) au kwa barua pepe brian@eriecriz.org ili kuanzisha mazungumzo au kupata majibu ya maswali yako.

## 16 Je, Mamlaka ya CRIZ huwa inatoa msaada wa kujaza na kuwasilisha taarifa zinazohitajika kwa Jumuiya ya Pennsylvania na kwa Jiji la Erie?

Ndiyo, Mamlaka ya Erie CRIZ imeajiri kampuni ya FourScore, LLC kuwasaidia wamiliki wa biashara na majengo kujaza na kuwasilisha taarifa zao za kila mwaka zinazohitajika kutumwa kwa Jumuiya na kwa Jiji bila malipo. Kampuni ya FourScore pia imeunda nyaraka za Excel ambazo zitakuwezesha kufuatilia mapato ya CRIZ kwa mwaka, na hivyo kufanya zoezi la kuwasilisha taarifa za mwaka kuwa rahisi. Kwa hiyo tafadhali wasiliana na timu ya FourScore kwa msaada wa bure katika kuwasilisha taarifa zako. Unaweza kuwafikia kupitia 484-951-1289 au kwa barua pepe Eriecrizcompliance@four-score.com.

# Eneo la Uhuishaji na Uboreshaji wa Jiji (CRIZ)

## Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara

FAQ

### 17 Ninatakiwa kuripoti nini, mwisho wa kuripoti ni lini, na kwa nini natakiwa kuripoti?

Chini ya sheria ya CRIZ, unatakiwa kuripoti kodi ambazo biashara yako tayari inazilipa na kuziripoti kwa mamlaka za jimbo na za mtaani kwako. Tafadhali anza kujaza fomu zako za taarifa za CRIZ mapema kabla ya tarehe ya mwisho ya kuwasilisha, ambayo ni Juni 15, 2026.

### 1 JIMBO Kodi za Jimbo la Pennsylvania (Idara ya Mapato):

| | | Ver el ejemplo |
|---|---|---|
| 1 | Fomu ya Ziada ya Mgawanyo wa Kodi (kama inahitajika) | APP |
| 2 | Kodi ya Mapato Halisi ya Kampuni * | CNI |
| 3 | Kodi ya Hisa za Benki * | BNK |
| 4 | Kodi ya Malipo ya Bima * | IPT |
| 5 | Kodi ya Mauzo na Matumizi – E-TIDES/Kodi ya Makazi ya Hotelini | SU & HO |
| 6 | Kodi ya Zuio la Mwajiri - Inahusisha Miradi ya CRIZ | Mradi wa EWH & EWH-CRIZ |
| 7 | Kodi ya Pombe Kali au Bia Inayokatwa na Mtengenezaji | MALT |
| 8 | Kodi ya Mauzo na Matumizi Inayolipwa na Mkandarasi kwa Ajili ya Vifaa vya Mradi Eneo la Mpango Huu | C-SU |
| 9 | Kodi ya Mauzo na Matumizi ya Majengo Binafsi au Huduma za Kushikika Zinazotumika na Biashara kwenye Eneo | TPP |
| 10 | Kodi ya Kupitisha ya PIT - Haijumuishi Mapato yasiyohusisha Utendaji wa Moja kwa Moja - Inajumuisha Miradi ya CRIZ | PIT |
| 11 | Jumla ya Kodi Inayohusishwa na Vinywaji vya Ngano au Pombe Zilizonunuliwa ili Kuuzwa tena kwenye Eneo la Mpango Huu (Ushuru na Kodi ya Mauzo) | MALT EX+SLS |
| 12 | Jumla ya Kodi Zinazohusika na Pombe Kali/Mvinyo Ulionunuliwa ili Kuuzwa Tena kwenye Eneo la Mpango Huu (Ushuru na Kodi ya Mauzo) | LIQR |

* Inategemea na Ugawaji. Kodi zingine zote hutumia Ugawaji huo.

### 1 MTAANI Kodi za Jiji la Erie:

| | | Tazama Mfano |
|---|---|---|
| 1 | Ujira wa Mwajiri wa Eneo lako | Mradi wa EIT & EIT-CRIZ |
| 2 | Kodi ya Mapato Yaliyopatikana | Mradi wa EIT & EIT-CRIZ |
| 3 | Kodi ya Huduma za Eneo Lako | Mradi wa LST & LST-CRIZ |
| 4 | Kodi ya Burudani | AMT |

# Eneo la Uhuishaji na Uboreshaji wa Jiji (CRIZ)

## Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara

F A Q

## 18 Wapi ninaweza kupakua Ripoti ya CRIZ ya Jimbo la Pennsylvania Idara ya Mapato?

Utaweza kuwasilisha ripoti kwa njia ya kuanzia Aprili 1 hadi Juni 15, 2026 kupitia:
https://www.eservices.revenue.pa.gov/NizCriz /Keystone/Session/Login

Hivi karibuni Idara ya Mapato imeanza kutumia mfumo wa usimamizi wa akaunti wa Keystone Login kwa ajili ya kufungulia ripoti ya Jimbo ya CRIZ. Mfumo uliokuwa ukitumika awali wa e-TIDES kwa ripoti za kila mwaka za CRIZ, umeondolewa rasmi. Kama bado haujafungua akaunti yako kwenye Keystone Login, utahitajika kujisajili kabla ya kutuma ripoti yako ya CRIZ ya mwaka huu. Baada ya kuziwasilisha na kabla haujatoka ndani ya mfumo, hakikisha unachapisha uthibitisho wa fomu zako za jimbo ulizowasilisha ili kuweka kwenye kumbukumbu zako.

## 19 Wapi ninaweza kupakua Taarifa ya CRIZ ya Mtaani kwangu?

Unaweza kupakua taarifa ya CRIZ ya Mitaa kwako kutoka kwenye tovuti ya Jiji la Erie hapa:
https://eriecriz.org

## 20 Utaratibu wangu wa kulipa kila kodi utabadilikaje?

Hautabadilika. Utaendelea kulipa Kodi zako za Jimbo na za Mtaani kwako kama ulivyozoea hapo awali. Programu ya CRIZ inachokutaka tu ukifanye ni kuwasilisha taarifa ya ziada inayoonyesha kodi ulizolipa kwa jimbo na kwa eneo lako ifikapo Juni 15 ya kila mwaka kwenye fomu wanazotoa.

## 21 Je, hii itamaanisha ninahitaji kufanya uhasibu zaidi? Na je, mhasibu wangu anaweza kunifanyia hili?

Hapana, hii haimaanishi utafanya shughuli za uhasibu za ziada. Utahitajika tu kutumia taarifa zako zilizopo tayari za biashara yako kuripoti kwenye fomu za kuwasilisha ripoti zako za kodi za CRIZ za Jimbo na za Mtaani kwako. Kumbuka, taarifa zinazoripotiwa ni za FEDHA TASLIMU iliyolipwa, kwa hiyo utahitaji rekodi za malipo yaliyofanywa au marejesho yaliyopokelewa kwa mwaka 2025 bila kujali ni ya mwaka gani. Mhasibu wako anaweza kukufanyia hili, hata hivyo, hakuna haja ya kuingia gharama za ziada ili kuwasilisha ripoti hizi. Kampuni ya FourScore imeajiriwa ili kukusaidia kujaza na kutuma fomu hizo BURE KABISA. Tafadhali wasiliana nao moja kwa moja ili kupata msaada kupitia Eriecrizcompliance@four-score.com au 484-951-1289.

## 22 Suala hili huenda likachukua muda mrefu. Nina muda kiasi gani kufanya hivi?

Kulingana na ugumu wa biashara yako, kujaza na kuwasilisha ripoti hizi inaweza kuchukua muda mfupi kama dakika tano au ikakuchukua muda mrefu kukusanya rekodi zako za malipo ya kodi zilizochaguliwa na kujaza fomu hizi. Timu ya wataalamu wa FourScore inaweza kukusaidia katika mchakato huu ili kupunguza muda utakaoutumia katika zoezi hili.

## 23 Je, watu wanaoishi ndani ya eneo la CRIZ wanatakiwa kufanya hili, pia?

Hapana. Watu binafsi ambao sio wamiliki wa biashara (sole proprietors) au watu ambao ni wapangaji wa makazi tu hawahitajiki kujaza na kuwasilisha ripoti hii. Erie CRIZ inachukua taarifa za kodi za biashara inayowasilisha ripoti husika, iwe ni mmiliki mmoja au taarifa za kodi za mmiliki wa jengo.